# SH'MINI ATZERET NI NINI?

Na Jacquelyn Fedor

Ilitafsiriwa Na William Obura

Sh'mini Atzeret ni sikukuu inayoadhimishwa sikuya 8, kuhesabu tangu mwanzo wa Sukkot au Hema. Ni sikukuu tofauti na Hema hata hivyo, na ni mkutano wake yenyewe, kusanyiko lake lenyewe.

**Walawi 23:36**

36 Kwa muda wa siku saba mtatoa sadaka anazo pewa Mwenyezi-Mungu kwa moto; **Siku ya nane** mtakuwa na **kusanyiko takatifu**, nanyi mtamtolea Mungu sadaka ya kuteketezwa. Ni **kusanyiko takatifu**, nanyi **hamtafanya kazi yoyote ya desturi juu yake**.

Sio watu wote wa Mungu watapata uzoefu wa Sh'mini Atzeret. Mwanadamu lazima akuze upendo na njaa ya Ukweli. Bila maarifa ya Mungu na ushiriki wa ndani katika mpango Wake wa urejesho hawawezi kuingia katika pumziko la Mungu kwani kwa ujinga watafuata ajenda zao wenyewe na kukataa mabadiliko. Kwa hivyo watabaki watoto wa siku ya 7.

Sh'mini ina maana ya 8. Nambari ya nane ni ishara ya mwanzo mpya, mzunguko mpya, enzi mpya. Kwa mfano, agano la tohara lilifanywa siku ya 8 kama ishara kwamba watu wa Mungu walikuwa katika uhusiano wa agano na Yeye na kwamba walimwamini Mungu kwa ajili ya ahadi alizompa

Ibrahimu kuhusu wakati ujao wa uzao wake.

Atzeret ina maana: "kuzuia" au "kile kilichozuiliwa" kwa madhumuni ya kuleta kitu kwenye hali ya ukamilifu. Ishara ya watu wa agano la Mungu leo ni tohara ya moyo na akili kutoka kwa ulimwengu na mifumo yake, kutenganisha kutoka kwa ujuzi wa ulimwengu hadi kwa akili ya Kristo, ujuzi wa Mungu, na kuweka chini ya kazi zao ili kufanya Yake. Mungu akiwa roho huona moyo na akili ya mwanadamu na ni wale tu waliotahiriwa wanaoingia katika pumziko Lake wanaweza kuingia katika agano la damu pamoja Naye ili wawe aina mpya, viumbe vipya kukaa katika dunia mpya.

Mavuno yalianza Rosh Hashanah.

**Ufunuo 14:14-16**

14 Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi
mmoja kama Mwana wa Adamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa
chake, na katika mkono wake mundu mkali.
15 Malaika mwingine akatoka Hekaluni, akimlilia kwa sauti kuu yule
aliyeketi juu ya lile wingu, akisema, **Tia mundu wako ukavune**; kwa maana
wakati umefika wa kuvuna, **kwa kuwa mavuno ya nchi yameiva**. "
16 Basi yeye aliyeketi juu ya wingu akautupa mundu wake juu ya nchi, nayo
nchi ikavunwa.

Zao hili la mwisho huamuliwa, kutiwa alama na ikichaguliwa kutengwa katika Rosh Hashanah kuwekwa katika nyumba ya Bwana kwa matumizi yake. Hawatachaguliwa tu bali watatayarishwa kama Mwili Wake. Ni wale ambao Mungu amemimina ukweli juu yao ambao wamekubali kwa urahisi neno au ufunuo ulioachiliwa kwa wakati huu wa mwisho. Ni hawa ambao wanaingizwa katika siku ya 8. Ukweli huu unaitwa "mvua ya masika". Imetolewa ili kulisha na kuleta uhai kwa siku ya 7 ya upandaji wa mwisho ambayo ilikomaa katika siku ya 8 kama zao maalum la Bwana. Picha ya mfano ilionyeshwa na Israeli ya zamani wakati wa sherehe ya Vibanda vilivyotabiri tukio hili. Ng'ombe-dume sabini walitolewa dhabihu kwa Mungu wakiwakilisha mataifa sabini tofauti-tofauti ya wanadamu ambako watu wake walitawanyika, lakini wakati wa Sh'mini Atzeret, fahali mmoja tu ndiye aliyetolewa dhabihu, akiwakilisha taifa moja, zao la pekee, Israeli mpya, aina mpya, ya Mungu. watoto wa agano. Huu ndio uzao wa kweli wa Ibrahimu ambao husherehekea sikukuu hii ya siku ya 8. Watoto wa siku ya 8 ni aina mpya na tofauti ya mbegu. Kizazi kilichoundwa kwa siku ya 8 ni tofauti sana kuliko kiumbe cha siku ya 7. Wao si wa Adamu tena, bali wamezaliwa kupitia kwa Mungu Mwenyewe!

**1 Petro 1:3-5**

3 Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi **alituzaa mara ya pili ili** tupate tumaini lililo hai kwa ufufuo wa Yesu Kristo katika wafu,

4 **tupate urithi usioharibika, usio na uchafu**. na **hiyo haififii**,
iliyohifadhiwa mbinguni (iliyoandikwa katika kitabu cha ukumbusho cha
Mungu) kwa ajili yenu,
5 **ambao mnalindwa na nguvu za Mungu** kwa njia ya imani hata mpate
wokovu ulio **tayari kufunuliwa wakati wa mwisho** (au mwisho wa
nyakati).

**I Yohana 5:18**

18 Twajua ya kuwa kila aliye **mtoto wa Mungu** hatendi dhambi; lakini yeye
aliye **mtoto wa Mungu** hujilinda, wala **yule mwovu hamgusi**.

Daudi alitabiri juu ya kutokea kwa kizazi hiki cha watu kwenye;

**Zaburi 102:18**.

18 Haya yataandikwa kwa **ajili ya kizazi kitakacho kuja**, ili watu ambao
**bado hawajaumbwa** (tofauti na wazao wa Adamu) wamsifu BWANA.

Mungu alimwahidi Abrahamu ngazi moja ya juu zaidi, ngazi ya "karibu zaidi na Mungu", watu maalum, taifa maalum, pamoja na ukuhani maalum. Hawa ni wale waliotiwa nuru kutoka katika pembe nne za dunia wanaojiweka safi na kufanya mavazi yao kuwa meupe. Tena, hili ni agano lililoingia kwa tohara siku ya 8, kwanza katika asili, na sasa katika ya ajabu kwa tohara ya moyo na akili. Watu hawa ni utimilifu wa ahadi za agano zilizotolewa kwa Ibrahimu. Wao ni watu waliowekwa kando, waliotakaswa ambao kwa

vyovyote si Adamu. Wao ni taifa lao la watu, waliojitenga na bado wapo wazi kwa watu wote ambao watazaliwa mara ya pili na kuvumilia tohara kutoka kwa yote yaliyo ya ulimwengu huu. Hawa ni wale waliositawisha uhusiano wa karibu sana na Mungu, na kuingia katika pumziko Lake ili kutimiza mpango Wake wa urejesho, kwa sababu walichagua kuwa sehemu ya Ufalme Wake.

Siku ya 8 watu, au wale wanaopata Sh'mini Atzeret, watadhihirisha ushindi wa Mungu juu ya adui. Kupitia kwao, jamii yao inapokua, falme za ulimwengu huu zitakuwa Ufalme wa Mungu wetu. Ulimwengu huu wa kimwili tunaoishi leo utafifia kutoka kwa macho. Malaki asema hivi:

**Malaki 4:1-3**

1 Kwa maana tazama, **siku inakuja**, inawaka kam tanuru, na wote, **wenye**
**kiburi**, ndio, **wote wafanyao uovu** watakuwa **makapi**. Na siku inayo kuja
(nyakati za mwisho) **zitawachoma**, “asema Bwana wa majeshi,” **ambao**
**atawaacha bila mzizi wala tawi**. (yote ambayo yametendeka kinyume na
mpango asili ya Mungu kwa urejesho wa binadamu yata haribiwa)
2 Lakini yule anaye liheshimu jina Langu, jua la haki litatokea na uponyaji
katika mabawa zake (urejesho na upya); na mtatoka na kuwa wanene kama
ndama waliohifadhiwa.
3 Utawakanyaga waovu maana **watakuwa kama majivu chini ya nyayo za**
**mguu wako** iyo **siku** **mimi nitakayo yafanya haya** asema bwana wa

majeshi.

Mapenzi ya Mungu ni muhimu zaidi kwa mtoto wa siku 8 kuliko watoto wake, kwa hivyo kazi zao ni zake. Ajenda yao kweli inakuwa Yake. Kwa hiyo, kukatishwa tamaa kwa kibinafsi kunakubaliwa kwa upole kama sehemu ya mpango wa Mungu wa kuwarejesha, kubadilisha asili zao za zamani, kusafisha mioyo na akili zao. Kuonekana kushindwa ni vyombo vya kuwatengeneza na kuwafinyanga katika sura yake na kuwaonyesha mwelekeo. Mlango uliofungwa wa fursa unamaanisha tu kuwa wako kwenye njia mbaya. Wanathamini Bwana kwa kufunga mlango na kuingilia kati kwa niaba yao na pia kwa ajili ya Ufalme. Hawa hawatazuiliwa na shida.

**Ufunuo 3:7-8**

7 “Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo yeyealiye mtakatifu, aliye wa kweli; **yeye aliye na ufunguo wa Daudi**, **yeye afunguaye** wala **hakuna afungaye** na **kufunga** na **hakuna afunguaye** (haya yanafanywa kwa kupenda kwake)":

8 "Nayajua matendo yako. Tazama, **nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako**, wala **hakuna awezaye kuufunga**; kwa maana unazo nguvu kidogo, umelishika neno langu, wala hukulikana jina langu.

Watu wa siku ya 8, wale wanaopata uzoefu wa Sh'mini Atzeret ni kanisa tukufu, kanisa lenye ushindi. Hakuna kinachoweza kuwashinda kwa sababu

Baba yao ana udhibiti wote na anawarudisha salama katika mpango Wake, katika pumziko Lake. Majina yao yamechorwa kwenye mkono Wake, akili zao na nyoyo zao ziko sawa, zikipatana Naye. Wanarudi kwa asili Yake, mfano wake, aliyeamuliwa kimbele kwa wakati huu, kizazi kipya, jamii tofauti ya watu waliozaliwa kupitia ukweli.

Watoto wa siku ya 8 hawaogope kuwa tofauti pia. Maandiko yanazungumza juu ya wakati ujao na walitambua kama watu wa siku ya 7 ambao walipaswa kubadili kuingia katika enzi hiyo. Hakuna kizazi kingine kilichokuwa kimeingia kikamili katika ahadi za Mungu! Je, kweli Biblia inazungumza kuhusu wakati ujao? Hapa kuna mifano michache tu.

**Mathayo 12:32**

32 "Yeyote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, lakini yeye atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa **katika wakati huu wala katika ule ujao**.

**Mariko 10:30**

30 "ambaye hatapokea mara mia sasa wakati huu nyumba na ndugu na dada na mama na watoto na mashamba pamoja na adha na **katika wakati ujao** uzima wa milele (uzima wa milele umo katika wakati ujao).

**Waefeso 1:21**

21 juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, si **katika wakati huu** tu, bali hata **katika ule ujao pia**.

Kama tunavyoweza kuona kutoka kwa maandiko, wakati ujao ni halisi sana na kama tulivyoona kutoka kwa maandiko, wale wanaoingia katika wakati huu watafanywa kuwa wa milele. Wakorintho wa Kwanza 15:51 itatimizwa ndani yao.

**1 Wakorintho 15:51-54**

51 Tazama, nawaambia ninyi siri: **Hatutalala sote** (hatutakufa), lakini sote **tutabadilishwa**,
52 kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho. Kwa maana tarumbeta italia, na wafu watafufuliwa wasiwe na uharibifu, nasi **tutabadilishwa**.
53 Maana sharti huu **uharibikao** uvae **kutoharibika,** nao huu **wa kufa** uvae **kutokufa.**
54 Basi huu uharibikao utakapovaa kutoweza kuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutoweza kufa, **ndipo litakapotimia lile neno lililoandikwa**: "**Kifo kimemezwa kwa ushindi**."

Mtoto wa siku ya nane hatakuwa tayari tu kutembea katika mipango ya Mungu, bali atatii kwa utii sheria alizoziandika kwenye akili na mioyo yao

hadi wawe sheria juu ya dhambi na uovu.

**Waebrania 8:10**

10 Maana hili ndilo agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli baada ya siku zile, asema Bwana; **Nitaweka sheria zangu akilini mwao** na **kuziandika moyoni mwao** nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.

Kwa hakika, wanapoingia katika pumziko la Mungu, wakiwarudisha kwenye mpango mkamilifu kwa ajili ya wanadamu, hata hawatazamii au kuona jambo baya, bali wataona mema tu. Tofauti na Adamu na Hawa, watakula tu matunda ya mti wa Uzima, na hawatatamani ladha ya matunda ya dunia au kutafuta ujuzi kutoka kwa Mti wa Mema na Uovu. Wao binafsi wamepitia taabu na kushindwa huko. Hawa watautazama Ufalme wa Mungu pekee. Hivi karibuni eneo hili, ulimwengu huu ambao umeibuka kupitia mwelekeo wa adui, utayeyuka au kutoweka machoni mwao, na hawatakuwa na kumbukumbu nalo. Yote ni mema katika ulimwengu wa Mungu: hakuna ugonjwa, hakuna maumivu, hakuna kushindwa nzuri tu na uzima wa milele. Ni ahadi nzuri kama nini kwa watoto wa siku ya 8! Ni jambo la kusisimua lililoje kwa wale walioalikwa kubaki mbele za Mfalme baada ya sikukuu ya hema!!

Hawa wa milele watatawala pamoja na Mungu miaka elfu moja, ambayo kwa Mungu ni siku moja tu, kuyazoeza mataifa. Wao ni mawe yaliyo hai

yanayofanyiza nyumba ya Mungu, mawe yaliyo hai yenye sheria iliyoandikwa kwenye mabamba ya nyama ya mioyo yao, hema ya Daudi. Watakuwa sheria iliyo hai kwa mataifa kwa sababu wao ni kimo kamili cha mwili wa Kristo. Yesu ndiye sheria, Torati na Roho wake hukaa na hujidhihirisha kupitia watoto wa siku ya 8 kuufundisha ulimwengu. Wale wanaochagua kufuata mwishoni mwa miaka elfu wataingia katika siku ya 9, wakifurahia Torah na wataadhimisha sikukuu ya mwisho na ya mwisho: Simchat Torah.

Nambari 9 inamaanisha nini? Karama za Roho Mtakatifu. Katika siku ya 9 vita vya mwisho vitakuwa vimepiganwa. Shetani, ambaye amefungwa kwa miaka elfu moja ataachiliwa ili kuwajaribu wale waliofunzwa katika ile miaka elfu moja, na hatimaye zawadi kubwa zaidi ambayo Roho Mtakatifu amewahi kumpa mwanadamu itaachiliwa kwa ajili ya wanadamu wengine ambao wamekuwa Torah: zawadi ya uzima wa milele na utawala kwa mara nyingine tena juu ya sayari hii! Utawala wa Shetani hatimaye utaharibiwa, pamoja na ulimwengu wake na jamii yake, utamaduni wake na raha, kwa kweli kuwepo kwake kote. Mwili wa Kristo, pamoja na mataifa wanaompenda, watapata ushindi na kufurahia sheria yake! Hebu tumalizie maono ya Danieli ya ushindi huu wa mwisho.

**Danieli 7:26-27**

26 'Lakini **mahakama itaketi**, nao **watamwondolea mamlaka yake**, **kuila**

**na kuuangamiza milele** (tunazungumza hapa juu ya Mpinga Kristo Shetani mwenyewe kupitia mwili wake).

27 **Ndipo ufalme na mamlaka**, na **ukuu wa falme** chini ya mbingu zote, **watapewa watu**, **watakatifu wake Aliye juu**. **Ufalme wake ni ufalme wa milele,** na mamlaka zote zitamtumikia na kumtii.

Kwa habari zaidi juu ya watoto wa siku ya 8, viumbe vipya, dunia mpya, walioalikwa kubaki kwa ajili ya sikukuu ya Sh'mini Atzeret, tunakutia moyo usome Kutekeleza Ushindi wa Kristo Duniani.

Tembelea tovuti yetu http://www.trumpetsoftruth.com